**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

## MWALIKO WA ZABUNI

**Kwa ajili ya:**

## MWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI KWA NJIA YA UBIA ILI KUJENGA NA KUENDESHA VYUMBA VYA BIASHARA ENEO LA MADUKANI KATA YA KIWIRA

**Tarehe: 29.09.2025**

1. **Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe** inawakaribisha mtu binafsi, kampuni, ushirika, Taasisi au kikundi cha watu kilichosajiliwa Kisheria kwa ajili ya Uwekezaji wa Sekta binafsi kwa njia ya Ubia. Ili kujenga na kuendesha vyumba kumi (10) vya biashara eneo la Madukani lililopo kata ya Kiwira ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

2. Mwombaji unakaribishwa kuleta zabuni yako **ya bei** kwa ajili ya ununuzi wa Zabuni kama ilivyoelekezwa kwenye Kitabu cha Zabuni na kama ilivyofafanuliwa katika kipengere cha ya Nne ya Tangazo hili.

3. Mwombaji mwenye nia na uwezo anaweza kufanya ziara ya kutembelea na kukagua eneo hilo ili kujua mahali mradi ulipo kwa gharama zake tarehe 01.10.2025 saa 4:00 Asubuhi. Baada ya hapo kutakuwa na kikao cha awali cha zabuni "Pre-bid meeting" kitakachofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri la Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, muda ni saa 08:00 Mchana ili kupata maelezo ya ziada ya Ubia kati ya Mwajiri na Mwekezaji.

4. Vitabu vya zabuni vitakuwa kwa Lugha ya **Kiswahili** vitanunuliwa na mwekezaji anayehitaji kwa gharama ambayo haitarudishwa ambayo ni Shilingi za kitanzania TSH.100,000/= (Laki moja tu) taslimu. Fedha hizo zilipwe Halmashauri ya Rungwe Ofisi ya Mapato. Vitabu vya zabuni vitatolewa Halmashauri ya wilaya ya Rungwe ofisi ya Ununuzi ghorofa ya Pili kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka 9:30 alasiri kwa siku za kazi tu.

5. Zabuni zote ziwe na nakala **halisi** (original) moja na **nakala** (Copy) moja inayofanana, iliyojazwa kwa usahihi na iliyowekwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na zitapokelewa na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni. Bahasha ziandikwe "**zabuni kwa ajili ya Uwekezaji wa Sekta binafsi kwa Njia ya Ubia ili kujenga na kuendeleza vibanda vya biashara eneo la Madukani kata ya Kiwira**"na kuwasilishwa kwa mkono kwa Anuani ifuatayo;

   **Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,**
   **Katibu wa Bodi ya Zabuni,**
   **Ofisi ya Manunuzi,**
   **S.L.P 148**
   **RUNGWE.**

6. Mwisho wa kuwasilisha zabuni ni Siku ya Jumatano **Tarehe** 08.10.2025 **kabla ya Saa 06:00 Mchana** Zabuni zote zitafunguliwa hadharani Tarehe 08.10.2025 Saa 06:00 Mchana mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa wawekezaji au wawekezaji walioamua kuhudhuria katika kikao katika

7. Zabuni zote lazima ziambatanishwe na tamko la kinga ya zabuni (Tender Securing Declaration) kwa mpangilio ulioelekezwa katika nyaraka za zabuni.

8. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielektroniki, na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa Zabuni, kwa hali yoyote ile hazitakubaliwa kwa tathimini.

…………………………
Mchau R,B.
**MKURUGENZI WA MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE